The Salvation Army
International Headquarters

101 QUEEN VICTORIA STREET
LONDON EC4V 4EH
Telephone: +[44] (20) 7332 8009
Fax: +[44] (20) 7332 8010
Email: IHQ-WM@salvationarmy.org

A Christian church and registered charity

OFFICE OF THE WORLD PRESIDENT
OF WOMEN'S MINISTRIES

Wapendwa Dada zangu,

Kama wafuasi wa Yesu, tumeitwa tuwe chumvi na nuru katika jamii zetu, tulete tumaini, uponyaji na mabadiliko kila tunako kwenda. Sauti ya Vita ni chombo kinachotafuta kuwawezesha na kuwahamasisha wanawake wajihusishe na utendaji wa haki ya jamii katika eneo lao, ni jibu letu kwa mwito wa Isaya 1:17: 'Jifunzeni kutenda mema, takeni hukumu ya haki, wasaidieni walioonewa, mpatieni yatima haki yake, mteteeni mjane.'

Jeshi la Wokovu wakati wote limekuwa nyumbani kwa wanawake wanaohusika na haki ya jamii na vitendo ambavyo kiuhalisia vinaigusa dunia. Namfikiria rafiki yangu huko New Zealand ambaye, amestaafu kazi ya uuguzi, anatafuta nafasi yake ya kuendeleza huduma yake ya kuwalea wale wenye mahitaji ya mwongozo wa bure kuhusu hukumu na msaada wa tiba. Namfikiria mwenye umri wa miaka 19 anayepambana na umaskini kati ya wenzi wake kwa kufanya shughuli za kuchangisha fedha zinazo shirikisha maduka katika eneo na vituo vya jamii. Wazo lake la kuingilia kati limewasaidia wanafunzi wengi wanawake. Mifano hii inatukumbusha nini kinawezekana kama wanawake wakitumia karama na ujuzi wao kwa wema mkubwa. Hili silo jambo jipya kwa wanawake wa Jeshi la Wokovu, lakini tuna wajibu wa kulea kwa makusudi, kutunza na kuongoza kazi hii ya huduma katika vizazi vyote. Hapa ndipo Sauti ya Vita inapoingilia!

Kuhusisha Sauti ya Vita ni kutambua hitaji la jamii – bila kujali lina ukubwa au udogo gani – na kujisikia umejitoa kuliitikia. Ni mwaliko wa kukusanya timu yako ya marafiki, wenzako, akina mama, mabinti na wajukuu pamoja, na kufikiria namna ya kutumika kama mlivyowekwa kipekee kundi la akina mama na kupewa karama. Fanya kazi kwa nguvu zako kama mshonaji, basi shona, kama unaweza kufundisha,basi fundisha, kama unaweza kupika, basi pika, kama unaweza kutengeneza mtandao, basi tengeneza mtandao. Tumia ujuzi wako kuunganisha watu zaidi ya maeneo yako ya kawaida. Nenda nje ya jengo la kanisa lako ukafanye jambo zuri kwa wengine, katika jina la Yesu!

Duniani, Jeshi lla Wokovu linatambua wajibu wa wanawake katika kukabiliana na maswala ya haki ya jamii. Hamu yetu ni kwamba, kupitia kwa misaada hii ya kwanza ya Sauti ya Vita, tutawaona wanawake wengi wakijitokeza kwenye mwito wao kama mawakala wa haki ya jamii. Mpango wa kujifunza neno la Mungu utatolewa katika miezi ijayo, na baadaye mwaka 2025, kozi za kwenye mtandao zitaelimisha na kuwawezesha wale ambao wanapenda kuchunguza majibu kuhusu haki. Tafadhali tufuate kwenye mtandao wa jamii na tutembelee kwenye webpage: salvationarmy.org/ihq/womensministries

Ingawa tunaweza kuwa na mashaka kama kujitoa kwetu kutaweza kutoa tofauti yoyote na inaweza kuonekana kuwa rahisi kuyaacha mambo kwa wataalamu, lazima tukumbuke kwamba, kama ilivyo njia ya Ufalme, kila mmoja ana sehemu ya kufanya. Anza kwa urahisi. Anza kidogo na kile unachokifahamu. Kila mara patakuwepo na mahali pa ngazi ya juu ya mafunzo na majibu ya kuratibiwa, lakini mchango wako ili kutengeneza dunia bora unahitajika. Sisi tuna nguvu zaidi pamoja.

Maombi yangu kwako ni haya: 'Mungu akubariki kwa kukufanya usiridhike na majibu rahisi, ukweli nusu, mahusiano bandia ili uishi kutoka ndani kabisa ya moyo wako. Mungu akubariki kwa kukupa hasira kuhusu ukosefu wa haki, ukandamizaji, na unyonyaji wa watu, ili ufanye kazi kutafuta haki, usawa na amani … Mungu akubariki kwa kukupa ujinga wa kufikiri unaweza kuleta tofauti duniani, ili uyafanye yale mambo ambayo wengine wanakwambia hayawezekani' (Sister Ruth Fox, 1985).

Nakualika ujiunge nasi katika kazi hii muhimu. Pamoja, na tuwe jasiri kupaza sauti kwa hekima na neema, na tuwe jasiri katika utafutaji wa haki.

Neema na amani kwako,

Bronwyn Buckingham

Kamishena
*Rais wa Huduma za Wanawake Duniani*